BENKI KUU YA TANZANIA



# Tathmini Ya Mwenendo Wa Uchumi

Juni 2026

Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia........................................1
2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa........................................3
2.1 Mfumuko wa Bei........................................3
2.2 Sera ya Fedha........................................5
2.3 Viwango vya Riba........................................7
2.4 Masoko ya Fedha........................................8
2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali........................................9
2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa........................................10
2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje........................................12
3.0 Mwenendo wa Uchumi Zanzibar........................................17
3.1 Mfumuko wa Bei........................................17
3.2 Bajeti ya Serikali........................................18
3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje........................................19
VIAMBATISHO........................................21

# 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia katika kipindi cha mwezi Mei 2026 umeendelea kukabiliwa na hali ya kutokuwa na uhakika, kutokana na mwenendo wa mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati (Kielelezo 1.1a na Kielelezo 1.1b). Mgogoro huo umeendelea kuvuruga uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa kutoka nchi za Ghuba ya Uajemi, na kupelekea bei za nishati na bidhaa nyingine muhimu kuendelea kuongezeka, hali inayoathiri imani ya wawekezaji, kupunguza kipato halisi cha kaya na kuongeza shinikizo la mfumuko wa bei duniani.

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Biashara Duniani**




Chanzo: https://worlduncertainityindex.com/

Kwa mujibu wa taarifa ya uchumi ya OECD ya Juni 2026, ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 2.8 mwaka 2026 (Kielelezo 1.2), licha ya kuimarika kwa masoko ya ajira, uwekezaji na maendeleo ya Akili Unde. Hatari kubwa inayoweza kusababisha kudorora zaidi kwa uchumi wa dunia katika siku za usoni ni uwezekano wa kuendelea kwa mgogoro katika eneo la Ghuba ya Uajemi, hali inayoweza kusababisha ongezeko kubwa la mfumuko wa bei duniani na hivyo kudhoofisha zaidi shughuli za kiuchumi.

**Kielelezo 1.2: Ukuaji Halisi wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi**

Asilimia




Chanzo: OECD Economic Outlook, Volume 2026 Issue I

Bei ya mafuta ghafi ilipungua kwa kiasi katika kipindi cha mwezi Mei 2026, ambapo wastani wa bei ya mafuta aina ya Brent ilishuka kutoka dola za Marekani 117.29 kwa pipa mwezi Aprili 2026 hadi dola za Marekani 107.14 kwa pipa mwezi Mei 2026. Licha ya kupungua, bei zilibaki juu zaidi ya viwango vilivyokuwepo kabla ya mgogoro kwa takriban dola za Marekani 63 kwa pipa mwishoni mwa mwaka 2025, baada ya kupanda kwa kasi kuanzia mwezi Februari 2026 kutokana na kufungwa kwa Mlango Bahari wa Hormuz, hali iliyopunguza uzalishaji na usafirishaji wa mafuta (Kielelezo. 1.3).

**Kielelezo1.3: Wastani wa Bei ya Mafuta Ghafi ya Brent kwa Mwezi**

Dola za Marekani kwa Pipa




Chanzo: U.S. Energy Information Administration (EIA), Europe Brent Spot Price FOB

Gharama kubwa za nishati ziliendelea kusambaa katika masoko mengine (Kielelezo 1.4). Bei za mbolea ziliendelea kuwa juu mwezi Mei 2026, ambapo mbolea aina ya urea iliuzwa kwa wastani wa dola za Marekani 771 kwa tani, na mbolea aina ya DAP (di-ammonium phosphate) kwa dola za Marekani 770 kwa tani, ikiakisi uhaba wa gesi asilia pamoja na kuvurugika kwa usafirishaji wa malighafi muhimu kutoka nchi za Ghuba ya Uajemi.

Bei za mafuta ya kula ziliendelea kupanda zaidi, ambapo mafuta ya soya yalipanda hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 1,775 kwa tani, kutokana na kuongezeka kwa gharama za malighafi na usafirishaji, pamoja na mahitaji makubwa ya mafuta ya dizeli inayotokana na mimea (biodiesel), huku bei ya mafuta ya mawese ilifikia dola za Marekani 1,140 kwa tani. Bei ya dhahabu iliendelea kuwa katika viwango vya juu kihistoria, ikiwa wastani wa dola za Marekani 4,587 kwa wakia troi, ikichagizwa na mahitaji ya rasilimali salama kutokana na mivutano ya kijiopolitiki. Aidha, bei za kahawa zilibaki kuwa chini ya viwango vya juu vilivyorekodiwa mwaka 2025, ambapo bei ya kahawa aina ya Arabika ilishuka kufikia dola za Marekani 6.95 kwa kilogramu kutokana na kupungua kwa vikwazo vya upatikanaji vilivyokuwepo awali.

**Kielelezo 1.4: Bei za Bidhaa Ulimwenguni**




Chanzo: www.worldbank.org/en/research/commodity-markets
Notes: DAP denotes Di-ammonium phosphate

Mwenendo wa bei za bidhaa katika masoko ya dunia uliendelea kuweka mfumuko wa bei duniani katika mwelekeo wa kupanda. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei wa jumla ulibaki tulivu, ingawa ulianza kuonesha dalili za kupanda kutokana na athari za kuongezeka kwa bei za nishati. Aidha, benki kuu za nchi hizo ziliendelea kuchukua tahadhari kwa kutobadilisha viwango vya riba ya sera za fedha hadi kufikia mwezi Mei 2026, huku zikionesha wasiwasi unaoongezeka kuhusu athari za mfumuko wa bei unaotokana na kupanda kwa gharama za nishati.

Mfumuko wa bei nchini Marekani uliongezeka na kufikia asilimia 4.2, ambapo sehemu kubwa ya ongezeko hilo ilitokana na kupanda kwa gharama za nishati, wakati katika nchi za Ukanda wa Sarafu ya Ulaya mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 3.2, ukichagizwa zaidi na bei za nishati pamoja na gharama za huduma. Mfumuko wa bei nchini Uingereza ulibaki katika kiwango cha asilimia 2.8.

Katika nchi za masoko yanayoibukia kiuchumi, mwenendo wa mfumuko wa bei ulitofautiana. Mfumuko wa bei nchini China ulikuwa asilimia 1.2 kutokana na udhaifu wa mahitaji ya ndani pamoja na kushuka kwa bei za chakula, aidha, kwa India mfumuko wa bei ulipanda hadi asilimia 3.9, kiwango cha juu zaidi katika kipindi cha miezi kumi na sita, ukichagizwa hasa na kupanda kwa bei za chakula pamoja na athari za taratibu za kupanda kwa gharama za nishati (Kielelezo 1.5).

**Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazochipukia Kiuchumi**



Chanzo: Bloomberg

Katika nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, shinikizo la mfumuko wa bei liliongezeka mwezi Mei 2026, ambapo baadhi ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) zilirekodi viwango vya juu zaidi, kwa kiasi ikiakisi athari za kupanda kwa bei za nishati na chakula katika soko la dunia (Kielelezo 1.6 na Kielelezo

1.7). Ingawa mfumuko wa bei katika nchi nyingi uliendelea kubaki ndani au karibu na lengo, mwenendo wa kuongezeka kwa bei za mafuta na mbolea katika soko la dunia kunaleta hatari kubwa ya mfumuko wa bei kuongezeka zaidi katika ukanda huu, hususan kwa nchi zinazotegemea uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje.

**Kielelezo 1.6: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**



**Kielelezo 1.7: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei uliongezeka kidogo mwezi Mei 2026, lakini ulibaki ndani ya lengo la taifa na vigezo vya mtangamano wa kikanda vya SADC na EAC. Mfumuko wa bei wa jumla ulifikia asilimia 4.2, kutoka asilimia 4.0 mwezi Aprili 2026 na asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.1). Ongezeko hilo lilitokana hasa na athari za kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, hali iliyopelekea gharama za usafiri na usafirishaji kupanda. Kwa kuzingatia kuendelea kwa mivutano ya kijiopolitiki na kisiasa duniani, matarajio ya mfumuko wa bei katika kipindi cha karibuni yanaendelea kukabiliwa na hatari zinazotokana na bei za bidhaa kutoka nje. Hata hivyo, upatikanaji wa kutosha wa chakula nchini pamoja na ruzuku ya mafuta iliyoanzishwa kati ya mwezi Aprili 2026 na Mei 2026 vinatarajiwa kupunguza makali ya shinikizo hilo.

**Jedwali 2.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei**

2020 = 100

| | | Badiliko la Mfumuko wa Bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiliko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiliko kwa Mwaka | | |
| Makundi Makuu ya Fahirisi | Mizania | Mei-25 | Apr-26 | Mei-26 | Mei-25 | Apr-26 | Mei-26 |
| Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 0.0 | 0.9 | -0.1 | 5.6 | 5.7 | 5.6 |
| Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 0.1 | 0.3 | -0.1 | 3.4 | 2.3 | 2.1 |
| Nguo, Mavazi na Viatu | 10.8 | 0.2 | 0.3 | 0.1 | 2.0 | 1.6 | 1.5 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | 0.2 | 0.9 | -0.8 | 3.4 | 1.7 | 0.7 |
| Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | 7.9 | 0.2 | 0.4 | 0.1 | 2.3 | 2.6 | 2.5 |
| Afya | 2.5 | 0.2 | 0.6 | 0.0 | 1.7 | 1.6 | 1.4 |
| Usafiri | 14.1 | -0.1 | 5.2 | 2.4 | 1.7 | 9.2 | 11.9 |
| Habari na Mawasiliano | 5.4 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 1.0 | 0.9 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 0.1 | 0.3 | 0.0 | 1.5 | 0.7 | 0.7 |
| Elimu | 2.0 | 0.0 | 1.6 | 0.1 | 3.2 | 2.6 | 2.7 |
| Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 0.2 | 0.1 | 0.3 | 1.8 | 1.8 | 1.9 |
| Bima na Huduma za Kifedha | 2.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.7 | 0.1 | 0.2 |
| Huduma Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidha na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 0.0 | 0.2 | 0.1 | 2.0 | 3.5 | 3.5 |
| Fahirisi Bidhaa Zote | 100.0 | 0.1 | 1.3 | 0.2 | 3.2 | 4.0 | 4.2 |
| Makundi Mengine Teule | | | | | | | |
| Faharisi ya Bidhaa za Msingi | 73.9 | 0.2 | 1.1 | 0.4 | 2.1 | 3.1 | 3.4 |
| Fahirisi Isiyojumuisha Fahirishi za Bidhaa za Msingi | 26.1 | -0.2 | 1.7 | -0.2 | 5.6 | 6.3 | 6.3 |
| Fahirisi za Mafuta, Nishati na Bili za Maji | 5.7 | 0.0 | 5.1 | -0.3 | 6.1 | 5.3 | 5.0 |
| Fahirisi za Huduma | 37.2 | 0.0 | 1.8 | 0.7 | 1.0 | 4.0 | 4.7 |
| Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | 0.1 | 1.0 | 0.0 | 4.2 | 4.0 | 4.0 |
| Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 0.0 | 0.7 | 0.1 | 3.2 | 1.4 | 1.5 |
| Fahirisi za Bidhaa zote Isipokuwa Chakula na Vinywaji Visivyo na Kilevi | 71.8 | 0.1 | 1.5 | 0.4 | 2.1 | 3.3 | 3.6 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.1.1: Mfumuko wa Bei na Malengo yake**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei wa msingi, ambao haujumuishi chakula ambacho hakijachakatwa na nishati, uliongezeka kufikia asilimia 3.4 mwezi Mei 2026, kutoka asilimia 3.1 iliyorekodiwa Aprili 2026 na asilimia 2.1 katika mwaka uliotangulia, ukichangiwa na bei za saruji, usafiri, samani, vifaa vya nyumbani na matunzo ya kawaida ya nyumba

(Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.2). Mfumuko wa bei wa msingi uliendelea kuwa na mchango mkubwa katika mfumuko wa bei wa jumla, ukichangia asilimia 2.6 mwezi Mei 2026 (Kielelezo 2.1.3).

**Kielelezo 2.1.2: Viwango vya Mfumuko wa bei kwa Miezi Kumi na Mbili**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

**Kielelezo 2.1.3: Mchango Katika Mfumuko wa Bei**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei za chakula ulipungua kidogo hadi asilimia 5.6 Mei 2026, kutoka asilimia 5.7 Aprili 2026, ukichangiwa na utulivu wa bei za mtama, ngano, ulezi, maharage na mahindi (Kielelezo 2.1.4a, na Kielelezo 2.1.4b). Bei za chakula zinatarajiwa kupungua, kutokana na kuanza kwa msimu wa mavuno mwezi Mei/Juni 2026 katika maeneo mengi nchini. Akiba ya chakula iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ilikuwa ya kutosha ikifikia tani 500,692 mwezi Mei 2026, baada ya kutoa tani 10,234.5 za mahindi na mpunga kwa wafanyabiashara katika mwezi husika (Jedwali 2.1.2).

**Kielelezo 2.1.4: Mabadiliko ya Mwaka ya Bei za Jumla za Mazao**

a. **Mazao ya Vyakula Vikuu**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

b. **Mazao ya Vyakula Mbadala**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

Tani

| Kipindi | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 | 567,469 |
| Feb | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 | 560,008 |
| Mac | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 | 533,634 |
| Apr | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 | 510,927 |
| Mei | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 | 500,692 |
| Jun | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 | |
| Jul | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 | |
| Ago | 144,410 | 210,020 | 489,187 | 537,571 | |
| Sep | 149,044 | 244,169 | 651,403 | 570,519 | |
| Okt | 151,794 | 244,289 | 708,399 | 593,485 | |
| Nov | 147,401 | 244,223 | 702,502 | 590,425 | |
| Des | 137,655 | 248,282 | 677,115 | 577,376 | |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula.

Mfumuko wa bei za nishati, mafuta na huduma za msingi ulikuwa kwa asilimia 5 mwezi Mei 2026, kutoka asilimia 5.3 mwezi April 2026 na asilimia 6.1 iliyorekodiwa katika mwezi kama huo mwaka 2025 (Jedwali 2.1.1). Pamoja na kupungua kwa

mfumuko wa bei, bei za rejareja za mafuta zimeendelea kuwa juu kutokana na athari za Mgogoro wa Mashariki ya Kati (Kielelezo 2.1.5).

**Kielelezo 2.1.5: Bei za Bidhaa za Mafuta**

Kwa lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Tanbihi: Bidhaa nyeupe za petroli huashiria wastani wa bei za Dunia

## 2.2 Sera ya Fedha

Utekelezaji wa sera ya fedha katika kipindi cha mwezi Mei 2026 uliendelea kuzingatia maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha (MPC), ambapo katika kikao chake cha mwezi Aprili 2026, Kamati ilibakiza Kiwango cha Riba cha Benki Kuu (CBR) katika asilimia 5.75 kwa robo ya mwaka inayoishia Juni 2026. Uamuzi huu ulilenga kuleta uwiano kati ya vihatarishi vya mfumuko wa bei na matarajio ya ukuaji wa uchumi.

Sambamba na uamuzi huo, utekelezaji wa sera ulilenga kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya mabenki (7-day IBCM) inabaki ndani ya wigo wa CBR, ambao ulipunguzwa kutoka asilimia 2.0 hadi asilimia 1.5 juu na chini ya kiwango hicho, ili kuboresha mwenendo wa viashiria vya sera.

Hatua hizo zilifanikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha katika mfumo wa mabenki, na hivyo kuchagiza ukuaji wa shughuli za kiuchumi kupitia ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi. Riba za muda mfupi katika soko la fedha ziliendana na mwelekeo wa sera, ambapo wastani wa riba ya siku saba baina ya mabenki ulikuwa asilimia 5.92 mwezi Mei 2026, ndani ya wigo uliowekwa (Kielelezo 2.2.1).

**Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa Siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Aidha, Benki Kuu iliendelea kusimamia kiwango cha ukwasi katika mfumo wa mabenki kwa kutumia mikopo ya muda mfupi (reverse repo). Mauzo yaliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 399.5 mwezi Mei 2026, kutoka shilingi bilioni 379.7 mwezi April 2026, ikiakisi utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga upatikanaji wa mikopo na ukuaji wa uchumi (Kielelezo 2.2.2).

**Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya Muda Mfupi Kwa Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 25.2, kutoka asilimia 22 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia. Ongezeko hili lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1).

Mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 23.2 kwa mwaka unaoishia Mei 2026, karibu sawa na asilimia 23.6 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.2.4 na Kielelezo 2.2.5), ukiakisi nafuu

ya hali ya ukwasi na kuimarika kwa mahitaji ya mitaji kwa wafanyabiashara na kaya, hali iliyochochea uwekezaji wa sekta binafsi na matumizi ya kaya.

### Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi Wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

| | Kiasi (Shiling bilioni) | | | Ukuaji kwa mwaka (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipengele | Mei-25 | Apr-26 | Mei-26 | Mei-25 | Apr-26 | Mei-26 |
| Rasilimali halisi za nje | 14,028.1 | 14,553.5 | 13,308.6 | 27.8 | -0.7 | -5.1 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 11,844.6 | 13,066.6 | 12,633.9 | 1.0 | 6.5 | 6.7 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 2,183.6 | 1,486.8 | 674.7 | --- | -37.7 | -69.1 |
| Rasilimali halisi za ndani | 39,313.4 | 50,538.4 | 53,495.3 | 15.2 | 30.7 | 36.1 |
| Madai rasmi ya ndani | 52,813.1 | 61,759.8 | 63,283.0 | 13.9 | 18.8 | 19.8 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | 8,019.7 | 10,659.9 | 10,858.0 | -4.5 | 30.2 | 35.4 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 39,792.0 | 47,919.3 | 49,034.6 | 17.1 | 23.6 | 23.2 |
| Rasilimali nyinginezo | -13,499.7 | -11,221.4 | -9,787.7 | 10.1 | -15.7 | -27.5 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 53,341.5 | 65,091.9 | 66,803.8 | 18.3 | 22.0 | 25.2 |
| Amana za fedha za kigeni | 13,543.4 | 14,989.0 | 15,428.5 | 24.9 | 8.3 | 13.9 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 39,798.1 | 50,102.9 | 51,375.3 | 16.2 | 26.9 | 29.1 |
| Amana zinginezo | 15,583.2 | 18,951.4 | 19,122.7 | 18.5 | 22.4 | 22.7 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 24,214.9 | 31,151.6 | 32,252.6 | 14.8 | 29.7 | 33.2 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko | 7,438.9 | 8,107.1 | 8,444.4 | 14.1 | 15.4 | 13.5 |
| Amana za hundi | 16,776.0 | 23,044.5 | 23,808.2 | 15.1 | 35.6 | 41.9 |
| Fedha za msingi (M0) | 11,800.7 | 15,670.5 | 15,640.3 | 6.8 | 31.9 | 32.5 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Mikopo kwa sekta ya uchukuzi na mawasiliano ilikua kwa asilimia 44.6, ikifuatiwa na biashara kwa asilimia 35 na kilimo kwa asilimia 30.9 (Jedwali 2.2.2). Wakati huo huo, mikopo kwa shughuli binafsi, ambayo kwa kiasi kikubwa hutumika kugharamia shughuli za wajasiriamali wadogo sana, wadogo na wa kati (MSMEs), iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote ya sekta binafsi iliyopo, kwa asilimia 34.7, ikifuatiwa na shughuli za biashara na kilimo zilizochangia asilimia 14.9 na 13.8, mtawalia (Kielelezo 2.2.6).

### Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi

Asilimia

| | Mei-25 | Jun-25 | Jan-26 | Feb-26 | Mac-26 | Apr-26 | Mei-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uchukuzi na mawasiliano | 24.1 | 21.3 | 50.0 | 48.7 | 43.3 | 44.2 | 44.6 |
| Biashara | 25.6 | 25.7 | 34.2 | 39.4 | 39.5 | 39.7 | 35.0 |
| Kilimo | 27.9 | 25.7 | 29.5 | 28.1 | 21.8 | 20.6 | 30.9 |
| Ujenzi | 13.6 | 13.7 | 17.8 | 18.9 | 20.7 | 17.7 | 25.4 |
| Shughuli binafsi | 22.9 | 20.8 | 91.4 | 103.9 | 78.4 | 39.7 | 20.0 |
| Uchimbaji Madini | 29.8 | 30.2 | 27.9 | 31.9 | 28.5 | 30.5 | 19.8 |
| Viwanda | 21.7 | 22.5 | 1.6 | 5.2 | 4.4 | 6.0 | 3.3 |
| Hoteli na migahawa | 7.3 | 2.5 | -7.7 | -8.5 | -4.9 | 4.2 | -2.9 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

### Kielelezo 2.2.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi

Asilimia




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2. 3 Viwango vya Riba

Viwango vya riba havikuwa na mabadiliko makubwa kwa mwezi Mei 2026, ambapo riba za mikopo na amana kwa pamoja zilipungua kwa kasi ndogo. Riba za mikopo zilipungua kidogo na kufikia asilimia 15.32, kutoka asilimia 15.33 mwezi Aprili 2026, ambapo riba za mikopo kwa wateja wakubwa (negotiated lending rates) zilipungua hadi asilimia 11.9, kutoka asilimia 12.56.

Kwa upande wa amana, riba zilipungua hadi asilimia 8.43 kutoka asilimia 8.54, na riba za amana kwa wateja wakubwa zilipungua hadi asilimia 11.25 kutoka asilimia 11.37. Sambamba na mwenendo huo, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 5.22, kutoka asilimia 5.50 mwezi April 2026 (Jedwali 2.3.1). Kupungua kwa tofauti kati ya viwango hivyo kunaashiria kuimarika kwa ufanisi katika upokeaji amana na utoaji wa mikopo (financial intermediation), jambo ambalo, sambamba na kupungua kwa viwango vya riba vya mikopo vinavyokubaliwa kwa mazungumzo, linatarajiwa kuboresha upatikanaji wa mikopo kwa biashara na kaya.

**Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa Benki za Biashara**

Asilimia

| | Mei-25 | Des-25 | Jan-26 | Feb-26 | Mac-26 | Apr-26 | Mei-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.52 | 3.02 | 2.94 | 2.98 | 2.89 | 2.91 | 2.85 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.18 | 15.24 | 15.10 | 15.11 | 15.11 | 15.33 | 15.32 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 15.96 | 15.46 | 15.49 | 15.41 | 15.45 | 15.31 | 15.38 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 12.99 | 12.38 | 12.25 | 12.19 | 12.21 | 12.56 | 11.90 |
| Riba za amana -jumla | 8.58 | 8.36 | 8.33 | 8.32 | 8.33 | 8.54 | 8.43 |
| Riba za amana (miezi 12) | 9.72 | 9.58 | 9.70 | 9.82 | 9.60 | 9.81 | 10.17 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 10.64 | 11.66 | 11.74 | 11.48 | 11.57 | 11.37 | 11.25 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 6.24 | 5.88 | 5.79 | 5.59 | 5.85 | 5.50 | 5.22 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.4 Masoko ya Fedha Soko la dhamana za Serikali

Soko la dhamana za serikali liliendelea kufanya kazi kwa ufanisi katika mwezi Mei 2026, ambapo dhamana za muda mfupi zilikuwa na mahitaji makubwa zaidi na hivyo kufidia upungufu wa uhitaji (undersubscription) uliojitokeza katika minada ya hati fungani (dhamana za muda mrefu) sambamba na uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi katika mfumo wa benki.

Benki Kuu ilifanya minada miwili ya dhamana za Serikali za muda mfupi (Treasury bills) zenye thamani ya shilingi bilioni 498.1. Minada yote miwili ilikuwa na mahitaji makubwa zaidi ya kiwango kilichotangazwa (oversubscription), ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 1,330.3 zilipokelewa, huku zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 499.8 zikikubaliwa. Kufuatia mwenendo huu, wastani wa riba za dhamana za Serikali ulipungua hadi asilimia 4.74 kutoka asilimia 5.06 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.4.1).

**Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Vilevile, Benki ilifanya minada ya hati fungani za miaka 15 na 20, kwa ajili ya kugharamia matumizi ya Serikali, zenye thamani ya shilingi bilioni 165.5 na shilingi bilioni 236.3, mtawalia. Minada hiyo ilivutia zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 324.9, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 235.1 kati ya hizo zilikubaliwa. Wastani wa riba za hati fungani za miaka 15 na 20 ulipungua kidogo na kufikia asilimia 10.39 na asilimia 10.43, mtawalia.

## Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya mabenki (IBCM) liliendelea kuwezesha usambazaji wa ukwasi baina ya mabenki, ambapo jumla ya mauzo katika soko yalifikia shilingi bilioni 1,732.7, ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,567.8 mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.4.2).

Mikopo ya siku 7 iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote kwa asilimia 63.8. Wastani wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki

ulipungua hadi asilimia 6.14 kutoka asilimia 6.26 mwezi Aprili 2026.

**Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Soko la fedha za kigeni

Hali ya ukwasi katika soko la jumla la fedha za kigeni (IFEM) ilikuwa ya kuridhisha, ikichangiwa na mapato ya fedha za kigeni hususan kutokana na mauzo ya dhahabu nje ya nchi. Kufuatia mwenendo huo, mauzo katika soko yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 119.3 mwezi Mei 2026, kutoka dola za Marekani milioni 64.6 mwezi Aprili 2026. Benki Kuu ilishiriki katika soko kwa mujibu wa Sera ya ushiriki katika Soko la Fedha za Kigeni kwa kuuza dola za Marekani milioni 44, ikilinganishwa na dola milioni 15.3 mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.4.3).

Licha ya kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni, Shilingi ya Tanzania ilishuka thamani dhidi ya dola ya Marekani kwa kiasi kidogo, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,616.88 kwa dola moja mwezi Mei 2026, ikilinganishwa na shilingi 2,612.46 mwezi uliotangulia. Hata hivyo, katika mwaka unaoishia Mei 2026 thamani ya shilingi iliimarika kwa asilimia 3.02 ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 3.82 kipindi kama hicho Mei 2025.

**Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2. 5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Katika kipindi cha mwezi Aprili 2026, Serikali ilikusanya shilingi bilioni 3,242.3 sawa na asilimia 7.1 juu ya lengo la mwezi. Kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 3,111.9 zilikusanywa na Serikali Kuu, sawa na asilimia 96 ya mapato yote, juu ya lengo kwa asilimia 7.2 ( Kiambatisho, Jedwali A2).

Mapato ya kodi yaliendelea kuwa imara yakifikia shilingi bilioni 2,690.6, juu ya lengo la mwezi kwa asilimia 10.2, ikiashiria athari chanya za maboresho yanayoendelea katika usimamizi wa kodi pamoja na kuongezeka kwa uzingatiaji wa ulipaji kodi. Utendaji wa makusanyo ya kodi ulichangiwa zaidi na kodi za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na kodi ya mapato. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 421.3, sawa na asilimia 8.7 chini ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 461.4 (Kielelezo 2.5.1).

**Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Aprili**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

Serikali iliendelea kuwianisha matumizi yake kuendana na mapato, ikirekodi jumla ya matumizi ya shilingi bilioni 3,457.2. Kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 2,696.6 zilitumika kugharamia matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 760.6 zikielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

**Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Aprili**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

## 2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) lilifikia dola za Marekani milioni 51,492.5 mwishoni mwa mwezi Mei 2026, likipungua kidogo kutoka kiasi kilichorekodiwa mwezi uliotangulia, kikichangiwa na kupungua kwa deni la nje na ndani. Kati ya kiasi hicho, asilimia 70.8 ilikuwa deni la nje (Kiambatisho, Jedwali A10).

### Deni la Nje

Deni la nje (linalojumuisha deni la Serikali na la sekta binafsi) lilipungua kidogo na kufikia dola za Marekani milioni 36,446.8 mwishoni mwa Mei 2026. Kati ya kiasi hicho, asilimia 81.1 ilikuwa deni la nje la Serikali, huku sehemu iliyobaki ikiwa ni deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.6.1).

Mikopo ya nje iliyopokelewa mwezi Mei 2026 ilikuwa dola za Marekani milioni 125.9, ambapo sehemu kubwa ilipokelewa na Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 189.4 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 140 zilitumika kufanya malipo ya mkopo mkuu.

Mashirika ya kifedha ya kimataifa yaliendelea kuwa wakopeshaji wakuu, yakichangia asilimia 57.5, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.6.2). Kiasi kikubwa cha mkopo uliotolewa kilikuwa kwa ajili ya urari wa malipo ya nje na bajeti (BoP na budget support) ikifuatiwa na mikopo kwa shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Kwa upande wa aina ya mikopo kwa sarafu, dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya (Euro) (Jedwali 2.6.3 na 2.6.4).

**Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji**

Dola za Marekani Milioni

| | Mei-25 | | Apr-26[r] | | Mei-26[p] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Serikali Kuu | 27,126.0 | 80.8 | 29,669.8 | 81.3 | 29,561.3 | 81.1 |
| Deni ambalo halijalipwa | 27,047.6 | 80.5 | 29,589.6 | 81.1 | 29,480.8 | 80.9 |
| Malimbikizo ya riba | 78.4 | 0.2 | 80.1 | 0.2 | 80.6 | 0.2 |
| Sekta binafsi | 6,456.4 | 19.2 | 6,836.4 | 18.7 | 6,885.5 | 18.9 |
| Deni ambalo halijalipwa | 5,851.2 | 17.4 | 6,519.0 | 17.9 | 6,558.9 | 18.0 |
| Malimbikizo ya riba | 605.2 | 1.8 | 317.4 | 0.9 | 326.6 | 0.9 |
| Mashirika ya umma | 3.8 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 3.8 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Malimbikizo ya riba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla ya deni la nje | 33,586.1 | 100.0 | 36,506.1 | 100.0 | 36,446.8 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

**Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji**

Dola za Marekani Milioni

| | Mei-25 | | Apr-26[r] | | Mei-26[p] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 19,007.7 | 56.6 | 20,950.1 | 57.4 | 20,946.3 | 57.5 |
| Deni ambalo halijalipwa | 18,973.9 | 56.5 | 20,926.4 | 57.3 | 20,922.6 | 57.4 |
| Malimbikizo ya riba | 33.8 | 0.1 | 23.8 | 0.1 | 23.7 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,426.0 | 4.2 | 1,561.5 | 4.3 | 1,558.5 | 4.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,347.6 | 4.0 | 1,481.3 | 4.1 | 1,477.9 | 4.1 |
| Malimbikizo ya riba | 78.4 | 0.2 | 80.1 | 0.2 | 80.6 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 12,086.2 | 36.0 | 13,319.0 | 36.5 | 13,279.7 | 36.4 |
| Deni ambalo halijalipwa | 11,693.6 | 34.8 | 13,049.6 | 35.7 | 13,002.0 | 35.7 |
| Malimbikizo ya riba | 392.6 | 1.2 | 269.4 | 0.7 | 277.8 | 0.8 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,066.2 | 3.2 | 675.6 | 1.9 | 662.3 | 1.8 |
| Deni ambalo halijalipwa | 887.5 | 2.6 | 651.3 | 1.8 | 637.1 | 1.7 |
| Malimbikizo ya riba | 178.7 | 0.5 | 24.3 | 0.1 | 25.2 | 0.1 |
| Jumla ya deni la nje | 33,586.1 | 100.0 | 36,506.1 | 100.0 | 36,446.8 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

**Sanduku 1: Muhtasari wa mapendekezo ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/27.**

Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/27 imepangwa kuwa shilingi 62.33 trilioni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.3 ikilinganishwa na bajeti ya 2025/26. Kati ya kiasi hiki, asilimia 74.2 ya bajeti itatokana na mapato ya ndani, ikionyesha juhudi zinazoendelea za kujitegemea kibajeti. Matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kujumuisha takriban asilimia 33 ya bajeti yote, huku kipaumbele kikiwa kukamilisha miradi na programu za maendeleo zinazoendelea. Bajeti ni ya mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050 (Dira 2050). Inaangazia kuimarisha uthabiti wa uchumi jumla, kuendelea na mabadiliko ya kimuundo yakijumuisha kupanua wigo wa kodi na matumizi ya mifumo ya kidigitali kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani, kuimarisha sekta za uzalishaji, na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara. Juhudi pia zinalenga katika kupanua huduma za kijamii na kuimarisha nidhamu ya fedha kupitia marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania (Sura ya 197), ikijumuisha kupunguza ukomo wa mkopo wa muda mfupi "overdraft" wa Benki Kuu kutoka asilimia 18 hadi 14 ya mapato halisi ya mwaka uliopita.

Ukomo wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2026/27 unatokana na dhana zifuatazo za uchumi jumla:
Makadirio ya ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 6.3 mwaka 2026;
Mfumuko wa bei kuwa ndani ya wigo wa asilimia 3 hadi 5;
Mapato ya ndani na ya kodi yanatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 17.1 na asilimia 13.7 ya Pato la Taifa, mtawalia;
Ukomo wa nakisi ya bajeti wa asilimia 3 ya Pato la Taifa; na
Akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya angalau miezi minne ya uagizaji bidhaa kutoka nje

Mwelekeo wa Bajeti ya Tanzania ya mwaka 2026/27 kwa ujumla unaendana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Kwa ujumla, bajeti za nchi za EAC zinalenga kudumisha utulivu wa uchumi mpana huku zikiendeleza mageuzi ya kimuundo na mabadiliko ya kiuchumi, kukuza ukuaji shirikishi, maendeleo ya rasilimali watu, uboreshaji wa miundombinu na maendeleo ya kijamii, pamoja na kuhakikisha usimamizi Thabiti wa sera za kibajeti ili kuboresha ustawi wa wananchi. Viashiria vya sera ya kibajeti vya nchi wanachama wa EAC kwa mwaka wa fedha 2026/27 vimewasilishwa katika Jedwali 2.5.1.

**Jedwali 2.5.1:2026/27 Viashiria vya kibajeti kwa Baadhi ya Nchi za Afrika Mashariki**

| | Kenya | Rwanda | Tanzania | Uganda |
|---|---|---|---|---|
| Jumla ya bajeti (Trilioni za sarafu ya ndani) | 4.8 | 7.8 | 62.3 | 84.4 |
| Jumla ya bajeti (Bilioni za USD) | 37.2 | 5.3 | 23.9 | 22.5 |
| Mapato ya ndani (% ya Pato la Taifa) | 17.4 | | 17.1 | 15.9 |
| Ambapo mapato ya kodi (% ya Pato la Taifa) | | 15.5 | 13.7 | 14 |
| Nakisi ya bajeti (% ya Pato la Taifa) | 5.5 | 4.8 | 2.9 | 6.9 |
| Ambapo ufadhili wa ndani (% ya Pato la Taifa) | 4.9 | | 1.2 | |

Chanzo: Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2026/27 na Hazina za Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

**Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa aina ya Matumizi, kwa Asilimia**

| Shughuli ya uchumi | Mei-25 | Apr-26[r] | Mei-26[p] |
|---|---|---|---|
| Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support) | 20.7 | 21.9 | 21.8 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 21.6 | 21.8 | 21.8 |
| Kilimo | 5.1 | 5.1 | 5.3 |
| Nishati na madini | 12.9 | 13.1 | 13.1 |
| Viwanda | 3.6 | 3.7 | 3.7 |
| Huduma za jamii na elimu | 20.4 | 18.9 | 19.0 |
| Fedha na bima | 4.2 | 4.3 | 4.3 |
| Utalii | 1.8 | 1.7 | 1.7 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 4.6 | 5.1 | 4.9 |
| Mengineyo | 5.2 | 4.4 | 4.4 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

**Jedwali 2.6.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu, kwa Asilimia**

| Sarafu | Mei-25 | Apr-26[r] | Mei-26[p] |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 66.6 | 63.0 | 62.9 |
| Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro) | 17.3 | 15.8 | 15.6 |
| Yuan ya China | 6.4 | 5.8 | 5.8 |
| Sarafu nyinginezo | 9.7 | 15.4 | 15.6 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la Ndani

Deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 39,257.3 mwishoni mwa Mei 2026, likiwa limepungua kidogo ikilinganishwa na kiwango kilichorekodiwa mwishoni mwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.6.1). Kupungua kwa deni la ndani la Serikali kulitokana zaidi na matumizi madogo ya Bakaa Hasi, ambayo yalizidi athari za ongezeko la deni lililotokana na ukopaji kupitia dhamana za Serikali (Jedwali 2.6.5 na Jedwali 2.6.6).

**Kielelezo 2.6.1: Deni la ndani la Serikali kuu**




Chanzo: Wizara ya Fedha
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa.

**Jedwali 2.6.5: Deni la ndani la Serikali kuu kwa Vyanzo vya Mikopo**

Shilingi Bilioni

| Nyenzo | Mei-25 Kiasi | Mei-25 Mchango (%) | Apr-26 Kiasi | Apr-26 Mchango (%) | Mei-26P Kiasi | Mei-26P Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dhamana za serikali | 29,984.6 | 85.2 | 33,438.1 | 85.0 | 33,610.9 | 85.6 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 2,022.6 | 5.7 | 1,518.7 | 3.9 | 1,562.8 | 4.0 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.5 | 135.7 | 0.3 | 135.7 | 0.3 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 27,774.8 | 78.9 | 31,783.7 | 80.8 | 31,912.3 | 81.3 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 5,216.6 | 14.8 | 5,897.6 | 15.0 | 5,646.4 | 14.4 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 5,198.2 | 14.8 | 5,897.6 | 15.0 | 5,646.4 | 14.4 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 35,201.1 | 100.0 | 39,335.8 | 100.0 | 39,257.3 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

**Jedwali 2.6.6: Deni la ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji**

Shilingi Bilioni

| Mkopeshaji | Mei-25 Kiasi | Mei-25 Mchango (%) | Apr-26 Kiasi | Apr-26 Mchango (%) | Mei-26P Kiasi | Mei-26P Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Benki za biashara | 10,138.2 | 28.8 | 11,052.2 | 28.1 | 11,149.8 | 28.4 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 7,158.2 | 20.3 | 7,706.3 | 19.6 | 7,455.1 | 19.0 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 9,203.9 | 26.1 | 10,426.4 | 26.5 | 10,441.4 | 26.6 |
| Kampuni za bima | 1,840.0 | 5.2 | 2,012.5 | 5.1 | 2,030.7 | 5.2 |
| Mifuko maalumu ya Benki Kuu | 616.3 | 1.8 | 798.4 | 2.0 | 798.4 | 2.0 |
| Wengine | 6,244.5 | 17.7 | 7,339.8 | 18.7 | 7,381.7 | 18.8 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 35,201.1 | 100.0 | 39,335.8 | 100.0 | 39,257.3 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na na wawekezaji wasio wakazi

Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 278.8 mwezi Mei 2026, kupitia utoaji wa dhamana za Serikali. Kiasi hiki kilijumuisha shilingi bilioni 128.6 za hati fungani za Serikali na shilingi bilioni 150.2 za hati za dhamana za muda mfupi za Serikali (Kielelezo 2.6.2). Kwa kipindi hicho, ulipaji wa deni la ndani ulifikia jumla ya shilingi bilioni 367.7, ikijumuisha shilingi bilioni 106.1 zilizolipwa kama marejesho ya deni la msingi na shilingi bilioni 261.6 kama malipo ya riba.

**Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Mwenendo wa sekta ya nje katika mwaka ulioishia Mei 2026 ulikabiliwa na changamoto zilizotokana na athari za mgogoro ya kijiopolitiki ya kimataifa na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya baharini. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 2,209.5 kutoka dola za Marekani milioni 2,090.8 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita (Jedwali 2.7.1), gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma ziliongezeka zaidi kuliko mauzo ya nje ikichangiwa na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na bei ya bidhaa katika masoko ya dunia.

Hata hivyo, akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa katika kiwango cha kuridhisha, ikifikia dola za Marekani milioni 5,538.8 mwishoni mwa Mei 2026 kutoka dola za Marekani milioni 5,136.7 mwaka uliopita. Ongezeko hili linaakisi uimara wa sekta ya nje katika kukabiliana na changamoto za kimataifa, kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya nje, hususan dhahabu na utalii, pamoja na kuendelea kwa utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa dhahabu. Kiwango cha akiba kilitosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa muda wa miezi 4.3 ya makadirio ya uagizaji, na hivyo kubaki juu ya lengo la kitaifa (Kielelezo 2.7.1).

### Jedwali 2.7.1 Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali

Dola za Marekani Milioni

| | | | | Mwaka ulioishia Mei | | | Mabadiliko ya asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei-25 | Apr-26 | Mei-26 | 2024 | 2025 | 2026p | |
| Urari wa bidhaa | -658.9 | -907.6 | -771.8 | -6,058.3 | -4,555.6 | -5,410.6 | 18.8 |
| Zilozouzwa nje* | 550.4 | 788.0 | 963.3 | 7,758.7 | 9,654.7 | 11,627.9 | 20.4 |
| Zilizonunuliwa nje | 1,209.4 | 1,695.6 | 1,735.1 | 13,817.0 | 14,210.2 | 17,038.5 | 19.9 |
| Urari wa huduma | 253.09 | 317.3 | 368.7 | 4,174.6 | 3,939.6 | 4,681.4 | 18.8 |
| Mapato | 520.1 | 587.9 | 647.5 | 6,499.4 | 7,051.5 | 8,051.5 | 14.2 |
| Malipo | 267.0 | 270.7 | 278.8 | 2,324.9 | 3,111.9 | 3,370.1 | 8.3 |
| Urari wa bidhaa na huduma | -405.8 | -590.3 | -403.1 | -1,883.7 | -615.9 | -729.2 | 18.4 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 1,070.5 | 1,376.0 | 1,610.8 | 14,258.2 | 16,706.2 | 19,679.4 | 17.8 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 1,476.3 | 1,966.2 | 2,013.9 | 16,141.9 | 17,322.1 | 20,408.6 | 17.8 |
| Urari wa malipo wa vitega uchumi | -158.2 | -132.6 | -136.9 | -1,674.0 | -2,001.5 | -1,830.7 | -8.5 |
| Yaliyoingia | 19.1 | 20.1 | 19.8 | 321.4 | 296.8 | 298.3 | 0.5 |
| Yaliyotoka | 177.4 | 152.7 | 156.6 | 1,995.4 | 2,298.3 | 2,129.0 | -7.4 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 32.9 | 38.9 | 55.3 | 649.7 | 526.5 | 350.4 | -33.4 |
| Iliyoingia | 77.1 | 94.9 | 111.4 | 1,316.9 | 1,103.2 | 996.8 | -9.6 |
| ambapo Serikali | 2.2 | 0.0 | 10.5 | 135.8 | 135.3 | 28.5 | -78.9 |
| Iliyotoka | 44.2 | 56.1 | 56.1 | 667.2 | 576.7 | 646.5 | 12.1 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | -531.1 | -684.0 | -484.7 | -2,907.9 | -2,090.9 | -2,209.5 | 5.7 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: LHS Inaashiria skeli ya mhimili wa kushoto; RHS, Inaashiria skeli ya mhimili wa kulia

## Mauzo ya nje

Mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 17.8 na kufikia dola za Marekani milioni 19,679.4 katika mwaka ulioishia Mei 2026, kutoka dola za Marekani milioni 16,706.2 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na mauzo ya dhahabu nje ya nchi, bidhaa za viwandani, pamoja na mapato yatokanayo na utalii, ambavyo kwa pamoja vilichangia asilimia 60.8 ya jumla ya mauzo ya nje.

Mauzo ya nje ya bidhaa yaliongezeka kwa asilimia 20.4 na kufikia dola za Marekani milioni 11,627.9 katika mwaka ulioishia Mei 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,654.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, yakichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku na kahawa (Kielelezo 2.7.2). Mauzo ya nje ya dhahabu yaliongezeka kwa asilimia 46.7 hadi kufikia dola za Marekani milioni 5,532.3 kutoka dola za Marekani milioni 3,771.5, yakichangiwa na bei nzuri katika soko la dunia pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani. Vivyo hivyo, mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani yaliongezeka kwa asilimia 38.3 hadi dola za Marekani milioni 2,009.3 kutoka dola za Marekani milioni 1,452.6, kutokana na ongezeko la mahitaji ya bidhaa za chuma na vioo kutoka nchi jirani.

Mauzo ya nje ya bidhaa asilia yaliongezeka kwa asilimia 12.8 hadi dola za Marekani milioni 1,639.7 katika mwaka ulioishia Mei 2026 kutoka dola za Marekani milioni 1,453.8 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na mauzo ya tumbaku, kahawa na pamba. Ongezeko la mauzo ya tumbaku lilichangiwa zaidi na ongezeko la kiasi kilichouzwa nje, wakati kahawa ilitokana na bei nzuri katika soko la dunia. Mauzo ya pamba, kwa upande mwingine, yalichangiwa na ongezeko la bei na kiasi cha mauzo. Kwa mwezi, mauzo ya nje ya bidhaa yaliongezeka kwa asilimia 75.0 na kufikia dola za Marekani milioni 963.3 mwezi Mei 2026 kutoka dola za Marekani milioni 550.4 zilizorekodiwa mwezi Mei 2025, yakichangiwa zaidi na ongezeko la mauzo ya dhahabu na bidhaa za viwandani.

### Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali

Mapato ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 14.2

